

Je una wasiwasi kuhusu mradi wa UNDP?

Kitengo Cha kuhakikisha kwamba kazi ya UNDP
inalinda jamii na mazingira
na kitengo cha kuwajibu washikadau

Utangulizi

Iwapo unaamini kwamba mradi wa UNDP umedhuru, au unaweza kukudhuru, jamii yako au mazingira, unaweza kuomba usaidizi kutoka kwa kitengo cha UNDP cha kuhakikisha kwamba kazi ya UNDP inalinda mazingira na/ama Kitengo cha UNDP cha kuwajibu washikadau.

Kitengo cha Kulinda jamii na Mazingira - Kinatoa majibu kwa maswali yanayohusu kazi ya UNDP kulinda jamii na mazingira

Kitengo cha SECU kinachunguza malalamiko kutoka kwa jamii zilizoathiriwa na mradi, na pia malalamiko kutoka kwa watu binafsi ambao wanaamini kwamba UNDP haijaweka ahadi yake ya kulinda jamii na mazingira. Pia kitengo hiki kinatoa mapendekezo na hatua zinazoweza kuchukuliwa kutatua mizozo. Hii inajumuisha, hasa, yasiyo ya kufuata na viwango vya kijamii na mazingira ya UNDP.

Kitengo cha kuwajibu washikadau – kinawasaidia wahasika kutatua mizozo

Kitengo cha SRM kina wasaidia washikadau walioathiriwa na mradi, wabia wa UNDP (serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, biashara) na wengineo, kutatua kwa pamoja mizozo yanayohusika na athari za miradi ya UNDP kwa jamii na mazingira.

Ni nani anaweza kuwasilisha malalamiko?

Malalamiko yanaweza kuwasilishwa na mtu yeyote au jamii inayoamini kwamba mazingira au ustawi wao unaweza kuathiriwa na mradi wa UNDP. Mwakilishi, kama vile asasi ya kiraia, anaweza kuwasilisha malalamiko kwa niaba ya jamii zilizoathiriwa. Watu ambao wamewasilisha malalamiko wanaweza kuziomba SRM na SECU kuzilinda majina na vitambulisho vyao.

Ni wapi unaweza kuwasilisha Ombi ?

Tafadhali wasilisha maombi na maswali yote kwa SECU kwa
secuhotline@undp.org.

Maombi kwa SRM yanaweza kuwasilishwa kupitia ofisi ya UNDP nchini mwako, au kwa timu ilioko kwenye makao makuu ya SRM kwa
stakeholder.response@undp.org.

Anwani ya ofisi ya UNDP nchini mwako, inaweza kupatikana kwenye tovuti ya UNDP ya www.undp.org.

Ni habari gani unaweza kujumuisha kwenye ombi lako?

Ni muhimu kutoa habari hizi kwenye ombi lako:

- Jina, anwani, nambari ya simu, au maelezo mengine kuhusu jinsi tunaweza kuwasiliana nawe
- Iwapo ungependa kitambulisho chako kiwekwe siri wakati tunapofanya uchunguzi
- Jina, eneo na aina ya mradi wa UNDP
- Jinsi unavyoamini umeathiriwa, au unaweza kuathiriwa na mradi wa UNDP
- Maelezo kuhusu juhudi zingine, ikiwemo juhudi za kutatua mzozo, ambazo umezichukua

Kwa habari zaidi

www.undp.org/secu-srm

www.undp.org/ses

project.concerns@undp.org